

**Environmental Management and Biodiversity conservation of Forests,
Woodlands, and Wetlands of the Rufiji Delta and Floodplain**

**Ripoti ya Mafunzo ya Kukusanya Mbegu za Miti
ya Kienyeji, Uhudumiaji na Utunzaji wa Miche
kwa Wanavijiji wa Rufiji, Mtanza Msona**

**Report of Native Tree Seed Collection and
Growing Course for Villagers in Mtanza Msona,
Rufiji (Swahili with English Summary)
15 – 24 Oktoba 2001**

H.P. Msanga na I.K. Singo



Technical report No. 23

December 2001

For more information please contact

Project Manager,

Rufiji Environment Management Project

P.O. Box 13513

Dar-es-Salaam, Tanzania

Tel: 44 Utete Rufiji Or 023-2402972 or 022- 2666088/0741 322366 Dar-es-Salaam

Email: remputel@bushmail.net or iucndar@epiq.or.tz

¹The Rufiji District Council implements Rufiji Environment Management Project with technical assistance from IUCN – The World Conservation Union, and funding from the Royal Netherlands Embassy.

Yaliyomo

Shukrani.....	ii
English Summary	iii
1 Utangulizi	1
2 Utekelezaji	2
3 Mapendekezo	4
4 Viambatanisho	5
4.1 Viambatisho 1: Mkataba Nr. REMP/4.0.21.2	5
4.2 Kiambatisho 2: Ratiba ya mafunzo	6
4.3 Kiambatisho 3: Fomu ya tathmini ya mafunzo	7
4.4 Kiambatisho 4: Nakala ya cheti	8
4.5 Kiambatisho 5: Orodha ya wanafunzi.....	9
4.6 Kiambatisho 6: Orodha ya mashirika au watu wanaoweza kushirikiana na MUMARU katika mafunzo ya kuzalisha miti	10

Shukrani

Sisi kwa niaba ya Mradi wa Taifa wa Mbegu za Miti (National Tree Seed Programme – NTSP) tuna toa shukrani zetu za dhati kwa Mradi wa kusimamia Mazingira Rufiji (MUMARU) kwa kutuchagua sisi kwa kufanya kazi hii muhimu ya kuandaa masomo na kufundisha wanavijiji 20 walioteuliwa. Tunatoa shukrani za pekee kwa Bi. Rose Hogan, Mshauri wa MUMARU kwa kubuni mafunzo haya na kufanya kazi kubwa ya kuandaa mkataba na kusimamia shughuli zote. Pamoja na kazi nyingi alizonazo, aliweza kutumia muda wa siku mbili kufika Mtanzamsoma na kukaa katika kambi ili apate kushiriki katika na kujadiliana na wakufunzi pamoja na wanafunzi jinzi masomo yalivyokuwa yakifanyika.

Tungependa kumshukuru Bw. Chande, Afisa Maliasili wa Wilaya ya Rufiji ambaye alikuja kumuwakilisha Mkurugenzi wa Maendeleo wa Wilaya ya Rufiji katika kufunga masomo na kutoa vyeti kwa wanafunzi waliohitimu. Kuacha shughuli zake zingine na kwenda Mtanza Msona inaonyesha anavyothamini umuhimu wa mafunzo hayo.

Bw. Ismail Bainga, Afisa wa Kilimo, Wilaya ya Rufiji amefanya kazi nzuri ya kuandaa vitendea kazi, kuandaa kambi na kuwaandaa wanafunzi. Amekuwa akikaa katika kambini na kushiriki katika shughuli zote kuanzia mwanzo hadi mwisho. Mr. Salum Mtou akiwa mwanakijiji wa Mtanza Msona amewahamasisha wanafunzi kuhusu umuhimu wa masomo yaliyokuwa yanafundishwa na kusisitiza kuwa wanayo bahati kwa kupata nafasi hiyo ambayo ni kwa faida yao na kwa maendeleo ya vijiji vyao kwa ujumla.

Tunamshukuru Bw Mbone Mwenyekiti wa Mtanza Msona kwa kukubali mafunzo yafanyikie katika kijiji chake na pia kutoa ulinzi wakati wa usiku. Mwisho tunawapongeza wanafunzi wote kwa juhudi zao za kuzingatia masomo hadi mwisho.

Ni matumaini yetu kuwa ushirikiano wa NTSP na MUMARU utazidi kuendelea na NTSP tuko tayari kutoa msaada wowote wa kitaalamu pale tutakapohitajika.

H.P. Msanga na I.K. Singo
Mradi wa Taifa wa
Mbegu za Miti
S.L.P. 373
Morogoro

Report on Training Course on Indigenous Tree Propagation for Villagers in Rufiji, Mtanza Msona 15th – 24th October 2001

English Summary

The main task was to design, conduct and prepare report on a ten-day practical Training Course on “Indigenous Tree Propagation for 20 villagers from Rufiji District” as specified in the syllabus attached to this report. The course methodology was conducted in a participatory approach with at least 80% of the course time dedicated to practical activities by participants.

Before starting the training course contract agreement was made and signed between the Rufiji Environment Management Project, REMP (contracting authority) and the National Tree Seed Programme, NTSP (contractor) Twenty participants (10 females and 10 males) were nominated by the village governments of the 4 selected villages: Mtanza msona, Mbunju Mvuleni, Twasalie and Taja. REMP supplied camping facilities, meals, transport, stationers and some training equipment. The following activities were carried out by the contractor:

- Training notes were prepared and binded in the form of a booklet (76 pages) They were written in simple Kiswahili and well illustrated by line drawings. Each participant was given a copy at the beginning of the course.
- A detailed day-by-day syllabus was prepared for 10 day course (See Appendix 4.1, Annex 5).
- A day-by-day timetable was prepared for the 10-day course (See Appendix 4.2). Each participant was given a copy at the beginning of the course. This was followed as much as possible through the course period.
- Materials such earth balls, banana fibre pots, bamboo pots, seeds, botanical specimens etc. were brought to the venue for demonstration purposes.
- Suitable propagation and regeneration sites were selected at Bizi Hamlet south of river Rufiji at Mtanza Msona. Participants were trained through discussions on criteria used to select this site.
- Demonstrations and practicals on subjects listed in the syllabus were based on low input methods affordable by individuals and communities.
- Kiswahili was used as the main language of training but also scientific and Kindengereko languages were used where necessary, especially for plant names.
- At the end of the course certificates were issued all 20 participants who successfully completed the training course. (See Appendix 4.4).
- A participatory evaluation of the course was conducted (See Appendix 4.3)
- Recommendations for improvement of future courses included:

1. **Observation:** This course was conducted in a participatory approach in which practicals took 80% and theory 20% of the course time. This was well appreciated by participants.

Recommendation: This approach should continue to be used in coming courses:

2. **Observation:** The duration of the course was only 10 days. This period was somehow short considering the subjects which were covered. During evaluation majority of the participants indicated that the period was short.

Recommendation: We recommended that next time when there is a similar course the duration should be 14 days.

3. **Observation:** Twenty participants for the whole Rufiji District are not enough to teach others and cause impact on tree planting activities.

Recommendation: Another course like this with another 20 participants should be organised at the same venue in June 2002.

4. **Observation:** Through discussions among participants and facilitators it was observed that participants are too localised. They have not had the chance of visiting other villages in Tanzania where they could have learnt on how other people handle tree seeds and raise seedlings.

Recommendation: REMP should organise a study tour for the 20 participants who attended this course. Recommended places to visit include:

- National Tree Seed Programme (NTSP), Morogoro
- Horticulture Unit of SUA, Morogoro
- Dodoma Environment Network (DONET), Dodoma
- Makini Women Group, Dodoma
- Handeni intergrated Agroforestry Project (HIAD), Handeni.
- Kilimanjaro Village Afforestation Project, Same
- Northern Zone Mangrove Project, Tanga

5. **Observation:** REMP staff may not be aware on how participants will apply the knowledge they obtained.

Recommendation: REMP staff (Field Officers) should make a follow up by visiting and advise participants in their villages. This may be done at an interval of 6 months starting from November 2001.

6. **Observation:** Participants were provided with almost everything for their subsistence during the course period. Nevertheless they complained of not being paid allowance for incidentals.

Recommendation: With this context we recommend that REMP should consider this matter and pay a pocket money of about Tsh 5,000 per day for each participant.

1 Utangulizi

Mradi wa usimamizi wa Mazingira Rufiji (REMP/MUMARU) umefanya kazi kubwa ya kuwahimiza wanakijiji wa Rufiji ili wapande miti kwa ajili ya kupata mahitaji yao pamoja na kutunza mazingira. Wanavijiji wameitikia wito huo lakini hawana ujuzi wa kukusanya mbegu za miti, kuanzisha bustani au kupanda miti. Kwa hivyo MUMARU imetambua jambo hilo na ikaamua kuwafundisha wawakilishi wa vijiji (wanawake 10 na wanaume 10) ili waweze kupata ujuzi na utaalamu husika. Matarajio ni kwamba wanafunzi hao watafundisha wanavijiji wenzao kwa vitendo na ushauri.

MUMARU imechagua Mradi wa Taifa wa Mbegu za Miti (NTSP) kuendesha masomo haya kwa sababu utaalamu wao kuhusu miti ya asili na pia kujenga mawasiliano kati ya wanavijiji na taasisi hiyo. Masomo yalifanyikia Mtanza Msona katika mazingira halisi ya washiriki. Hivyo ilikuwa rahisi kutumia mifano ya miti, udongo, na vifaa vilivyopo.

Mbinu za asili zilizingatiwa kwa sababu zinagharama ndogo sana, zinaeleweka na wenyeji, na hazina madhara kwa mazingira. Mbinu za kisasa zilichanganywa na zile za asili pale ilipobidi. Sisi wakufunzi pia tulijifunza kutoka kwa wanafunzi katika majadiliano ya kuhusu mbinu mbali mbali mpaka kupata mbinu za kufaa katika mazingira ya Rufiji.

Mafunzo yote yalikazia kujifunza kwa vitendo (80%) na kujifunza kwa nadharia (20%). Mafunzo yalizingatia uwekezaji mdogo ambao wanavijiji wanaweza kutekeleza kwa mtu mmoja au kifamilia.

Bw. H.P. Msanga na Bw. I.K. Singo wakufunzi kwa kushirikiana na Bi. Rose Hogan wametayarisha kitabu ambacho kitakuwa mwongozo kwa wanafunzi wakiwa wanafundisha wenzao. Tunatumaini kuwa yeyote anayetaka kutunza na kuotesha miti ataazima kitabu hicho kutoka katika maktaba ya mazingira ya wilaya au Mtendaji Kata au Mratibu Elimu Kata, au vituo vya waalimu au maktaba za vijiji vya mfano Twasalie, Jaja, Mtanza Msona na Mbunjumvuleni.

2 Utekelezaji

Kazi hii ilihusu kuendesha mafunzo na hatimaye kuandika ripoti ya utekelezaji kwa kuzingatia kanuni za mkataba (Tazama kiambatanisho Nr. 4.1). Mafunzo yalitolewa kwa wanafunzi 20 (10 wanawake na 10 wanaume) kwa njia ya majadiliano kati ya wakufunzi na wanafunzi. Mafunzo kwa vitendo yalichukua muda kiasi cha 80% na kwa nadharia 20%. Wanafunzi walichaguliwa na serikali kutoka vijiji 4 vya mfano: Twasalie, Taja, Mbunjumvuleni na Mtanza Msona (Tazama kiambatanisho Nr. 4.5). REMP walitoa vifaa vya kujengea kambi; chakula kwa wakufunzi na wanafunzi, usafiri, karatasi, ulinzi na vifaa vya bustani.

Zifuatazo ni shughuli zilizofanyika:

- Kutayarisha kitabu cha kufundishia. Kitabu hiki kiliandikwa kwa lugha rahisi ya kiswahili na pia kina michoro mingi ya kumwezesha msomaji aelewe kwa urahisi. (Tazama kiambatanisho Nr. 4.8). Kila mwanafunzi alipatiwa nakala moja siku ya kwanza ya mafunzo.
- Kutayarisha mitaala (syllabus) ya mafunzo (Tazama kiambatanisho Nr. 4.1 kifungu Nr. 5).
- Kutayarisha ratiba ya kila siku ya mafunzo (Tazama kiambatanisho Nr. 4.2).
- Vitendea kazi vya maonyesho vilitayarishwa na wakufunzi na kuletwa katika eneo la kufundishia. Viriba vya udongo, viriba vya majani ya mgomba, viriba vya mianzi, mbegu za miti (Mkongo, Mchongoma, Mlonge, Mkenge, Mgunga) na sampuli za mimea.
- Sehemu inayofaa kwa kuanzishia bustani ilichaguliwa katika kitongoji cha Bizi, kusini mwa mto Rufiji katika kijiji cha Mtanza Msona. Wanafunzi walifundishwa kwa njia ya majadiliano vigezo vilivyotumika katika kuchagua eneo hilo.
- Maonyesho na mafunzo kwa njia ya vitendo ambayo yameorodheshwa katika mitaala yalizingatia uwekezaji usio na gharama kubwa, ambao mtu binafsi au wanavijiji wanaweza kutekeleza.
- Baada ya kumaliza mafunzo wanafunzi walishirikishwa katika kutathmini yale waliyofundishwa (Tazama kiambatanisho Nr. 4.3).
- Vyeti vilitolewa kwa kila mwanafunzi aliyehitimu (Tazama kiambatanisho Nr. 4.4).
 - Wanafunzi walifundishwa kwa vitendo kufanya mambo yafuatayo:
 - Kukadiria uwingi wa mbegu kabla ya kuvuna kwa mti wa Mfumbili
 - Kuvuna mbegu za Mtanga (*Albizia Versicolor*) Mtonge (*Strychnos cocculoides*), Mmoyomoyo (*Deenbolia borbonica*)
 - Kubangua na kusafisha mbegu kutoka katika matunda ya miti iliyotajwa hapo juu.
 - Kuchagua eneo la bustani.
 - Kutengeneza sanduku la kuoteshea mbegu
 - Kuanzisha bustani ya miche
 - Kutengeneza kitalu, tuta la miche, tuta la Swaziland,
 - Kutengeneza viriba vya udongo, majani ya mgomba, mianzi, makopo, mifuko ya nailoni na chupa za plastic.

REMP Technical Report 23: Tree Seeds Workshop

- Kutayarisha mchanganyiko wa udongo na kujaza viriba
- Kuhudumia mbegu kabla ya kuzisia kwa kutumia: maji baridi, maji ya moto, msasa, mkasi wa kucha, moto, waya wa moto n.k mbegu zilizotumika ni za Mkongo. Mtanga, Mgunga na Glirisidia.
- Kusia mbegu za Mkongo, Mtanga na Mgunga.
- Kubebesha miche.
- Kukatia miche.
- Kuzalisha miche kwa kutumia pingili.
- Kung'oa maotea.
- Kuchimba mashimo na kupanda miti.

3 Mapendekezo

1. **Kilichoonekana:** Haya mafunzo yaliendeshwa kwa njia ya majadiliano miongoni mwa wanafunzi wenyewe pamoja wawezeshaji ambapo kujifunza kwa vitendo kulichukua 80% ya muda na nadharia ilichukua 20%. Mtindo huu ulipendwa sana na wanafunzi.

Pendekezo: Mtindo huu uendelee kutumika kwa mafunzo yatakayofuata.

2. **Kilichoonekana:** Muda wa mafunzo ulikuwa siku 10 tu muda huu ulionekana kuwa mfupi ukilinganisha na masomo ambayo yalifundishwa. Wakati wa tathmini wanafunzi walio wengi nao waliona hivyo.

Pendekezo: Tunapendekeza kuwa hapo baadaye wakati wa kuandaa mafunzo kama haya muda uongezwe hadi siku 14.

3. **Kilichoonekana:** Wanafunzi 20 kwa Wilaya nzima ya Rufiji ni wachache mno, hawatoshi kuwafundisha wanavijiji wenzao na kuonyesha mabadiliko ya kupanda miti katika Wilaya.

Pendekezo:- Mafunzo mengine kama haya ni wanafunzi wengine 20 yaendeshwe mahali pale pale (Mtanzi Msona) Mwezi Juni 2002.

4. **Kilichoonekana:** Kwa njia ya majadiliano miongoni mwa wanafunzi wengi hawajapata fursa ya kuona jinsi wanavijiji au watu wengine wanavyo kusanya mbegu, kutunza bustani au kupanda miti.

Pendekezo: MUMARU waandae safari ya kujifunza (Study tour) kwa wanafunzi wote 20 waliofuzu mafunzo haya. Sehemu tunazopendekeza ni kama ifuatavyo:-

- Mradi wa Taifa wa Mbegu za Miti, Morogoro
- Kitengo cha mboga mboga na matunda cha Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine, Morogoro.
- Dodoma Environment Network (DONET), Dodoma.
- Makini Women Group, Dodoma.
- Handeni Intergrated Agroforestry Project (HIAD), Handeni.
- Kilimanjaro Village Afforestation Project, Same
- Himo Agroforestry Project, Himo
- Northern Zone Mangrove Project, Tanga

5. **Kilichoonekana:** Wafanyakazi wa MUMARU wanaweza wasifahamu jinsi wanafunzi watakavyotumia elimu waliyoipata.

Pendekezo: Wafanyakazi wa MUMARU wafuatilie kwa kuwatembelea wanafunzi na kuendelea kuwashauri jinsi ya kutekeleza yale waliyofundishwa shughuli hii inaweza ikafanyika kila baada ya miezi 6 kuanzia Novemba 2001.

6. **Kilichoonekana:** Wanafunzi walipatiwa karibu kila kitu kwa ajili yakuweza kuishi kambini wakati wa mafunzo. Hata hivyo walilalamika kwa kutokupewa posho ya vitu vya dharura.

Pendekezo:- Kutokana na maelezo hayo tunapendekeza kuwa MUMARU ifikirie jambo hili ikiwezekana katika mafunzo yajayo iwapo wanafunzi wapewe pesa za mfuko kama 5,000/= hivi kwa siku kwa kila mwanafunzi.

4 Viambatanisho

4.1 Viambatisho 1: Mkataba Nr. REMP/4.0.21.2.

4.2 Kiambatisho 2: Ratiba ya mafunzo

Tarehe	Wakati (saa)	Somo	Muwezeshaaji (Facilitator)
Jumatatu	3 - 7	<ul style="list-style-type: none"> Kutambua majina ya miti yenye manufaa 	Msanga
15/10/2001	7 - 8	<ul style="list-style-type: none"> Kupanga jinsi ya kuvuna mbegu 	Singo
	8 - 11	Mapumziko	
	3 - 7	<ul style="list-style-type: none"> Usajili wa mbegu 	Singo
Jumanne	3 - 7	<ul style="list-style-type: none"> Kuvuna mbegu 	Singo
16/10/2001	7 - 8	Mapumziko	
	8 - 11	<ul style="list-style-type: none"> Kuvuna mbegu 	Singo
Jumatano	3 - 7	<ul style="list-style-type: none"> Kubangua na kusafisha mbegu kavu 	Msanga
17/10/2001	7 - 8	Mapumziko	
	8 - 11	<ul style="list-style-type: none"> Kubangua na kusafisha mbegu teketeke 	Msanga
Alhamisi	3 - 7	<ul style="list-style-type: none"> Kupima ubora wa mbegu 	Msanga
18/10/2001	7 - 8	Mapumziko	
	8 - 11	<ul style="list-style-type: none"> Kuchagua eneo la kuanzishia bustani (nadharia) 	Singo
Ijumaa	3 - 7	<ul style="list-style-type: none"> Kuchagua eneo la kuanzishia bustani (vitendo) 	Singo
19/10/2001	7 - 8	Mapumziko	
	8 - 11	<ul style="list-style-type: none"> Kutengeneza kitalu (seed bed) na tuta la miche (seedling bed) 	Msanga
Jumamosi	3 - 7	<ul style="list-style-type: none"> Kuhudumiwa mbegu kabla ya kusia 	Msanga
20/10/2001	7 - 8	Mapumziko	
	8 - 11	<ul style="list-style-type: none"> Kusia / kuotesha mbegu 	Msanga
Jumapili	3 - 7	<ul style="list-style-type: none"> Kutayarisha mchanganyiko wa udongo 	Msanga
21/10/2001	7 - 8	Mapumziko	
	8 - 11	<ul style="list-style-type: none"> Kutengeneza viriba vya aina mbalimbali 	Singo
Jumatatu	3 - 7	<ul style="list-style-type: none"> Kujaza viriba na kupandikiza miche 	Singo
22/10/2001	7 - 8	<ul style="list-style-type: none"> Kuotesha pingili (vegetative propagation) 	Msanga
	8 - 11	Mapumziko	
	3 - 7	<ul style="list-style-type: none"> Kubebesha miche (grafting / buding) 	Singo
Jumanne	3 - 7	<ul style="list-style-type: none"> Kuzuia magonjwa na wadudu 	Msanga
23/10/2001	7 - 8	<ul style="list-style-type: none"> Kulea miche katika bustani 	Msanga
	8 - 11	Mapumziko	
	3 - 7	<ul style="list-style-type: none"> Kulea miche katika bustani 	Msanga
Jumatano	3 - 7	<ul style="list-style-type: none"> Kusafirisha miche 	Singo
24/10/2001	7 - 8	<ul style="list-style-type: none"> Gharama za bustani 	Singo
	8 - 10	<ul style="list-style-type: none"> Kuweka kumbukumbu 	Singo
	7 - 8	Mapumziko	
	8 - 10	<ul style="list-style-type: none"> Tathmini (Evaluation) 	Msanga Singo Rose Kilimba Bainga

4.3 Kiambatisho 3: Fomu ya tathmini ya mafunzo

Tathmini (Evaluation)

**MAFUNZO YA UVUNAJI MBEGU ZA MITI YA KIENYEJI,
UHUDUMIAJI NA UTUNZANI WA MICHE KWA WANAVIJIJI WA RUFJI
15 – 24 OKTOBA 2001**

Somo	Muwezesaji (Facilitator)	Tathmini (Evaluation)		
• Mwaliko	REMP	😊	😐	😞
• Mapokezi	REMP	😊	😐	😞
• Malazi	REMP	😊	😐	😞
• Maandalizi ya masomo	Msanga Singo	😊	😐	😞
• Kutambua majina ya miti	Msanga	😊	😐	😞
• Kupanga jinsi ya kuvuna mbegu	Singo	😊	😐	😞
• Kuvuna mbegu	Singo	😊	😐	😞
• Kubangua na kusafisha mbegu	Msanga	😊	😐	😞
• Kupima ubora wa mbegu	Msanga	😊	😐	😞
• Kuchagua eneo la kuanzisha mbegu	Singo	😊	😐	😞
• Kutengeneza kitalu	Msanga	😊	😐	😞
• Kuhudumia mbegu	Msanga	😊	😐	😞
• Kusia mbegu	Msanga	😊	😐	😞
• Kutayarisha mchanganyiko wa udongo	Singo	😊	😐	😞
• Kutengeneza viriba	Singo	😊	😐	😞
• Kujaza viriba na kupandikiza miche	Singo	😊	😐	😞
• Kuotesha pingili	Msanga	😊	😐	😞
• Kubebesha miche		😊	😐	😞
• Kuzuia magonjwa na wadudu	Msanga	😊	😐	😞
• Kulea miche katika bustani	Msanga	😊	😐	😞
• Kusafirisha miche	Msanga	😊	😐	😞
• Kupanda miti shambani	Msanga	😊	😐	😞
• Gharama za bustani	Singo	😊	😐	😞
• Kuweka kumbukumbu	Singo	😊	😐	😞

😊 Vizuri

😐 Wastani

😞 Vibaya

- Muda wa masomo ulikuwa:

Mfupi

Wakutosha

Mrefu mno

- Maoni mengine kama unayo

4.4 Kiambatisho 4: Nakala ya cheti

UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
National Tree Seed Programme

4.4 Nakala ya cheti



CERTIFICATE OF PARTICIPATION

This is to certify that

----- Sophia A. Ukwama -----

has participated in the **NTSP** training course on

(Indigenous tree propagation)
Uvunaji mbegu za miti ya kienyeji
Uhudumiaji na utunzaji wa miche

held at Mtanzamsona - Rufiji

during the period 15 - 24 October 2001

topics covered were

- * Tree seed harvesting
(Uvunaji wa mbegu za miti)
- * Seed processing
(Kubangua mbegu)
- * Nursery management
(Kutunza bustani)
- * Tree planting
(Kupanda miti)

Programme Coordinator

Programme Manager

4.5 Kiambatisho 5: Orodha ya wanafunzi

Jina la mwanafunzi	Jinsi	Kijiji alikotoka
1. Zajila J. Kitanda	Ke	Twasalie
2. Swaumu I. Kisoma	Ke	Twasalie
3. Amanu M. Kongwe	Me	Twasalie
4. Muhalami O. Mchomboye	Me	Twasalie
5. Rukia B. Muki	Ke	Jaja
6. Maimuna N. Bofu	Ke	Jaja
7. Bakari S. Mkumbi	Me	Jaja
8. Bakari H. Amagae	Me	Jaja
9. Sophia A. Ukwama	Ke	Mbunjumvuleni
10. Sophia R. Ndundu	Ke	Mbunjumvuleni
11. Juma S. Mtambo	Me	Mbunjumvuleni
12. Moshi M. Jongo	Me	Mbunjumvuleni
13. Saijali T. Mpako	Ke	Mtanza Msona
14. Tabia R. Mpitu	Ke	Mtanza Msona
15. Amana K. Nganywana	Ke	Mtanza Msona
16. Kulwa I. Mbonde	Ke	Mtanza Msona
17. Idadi J. Manyema	Me	Mtanza Msona
18. Amiri K. Mbena	Me	Mtanza Msona
19. Shabani K. Nduli	Me	Mtanza Msona
20. Ally S. Ngondo	Me	Mtanza Msona

Me = Mwanamme

Ke = Mwanamke

4.6 Kiambatisho 6: Orodha ya mashirika au watu wanaoweza kushirikiana na MUMARU katika mafunzo ya kuzalisha miti

- 4.6.1 Bw. H.P. Msanga/Bw. I.K. Singo/Bw. C.K. Ruffo
Mradi wa Taifa wa Mbegu za Miti
S.L.P. 373
Morogoro
Simu: 023 3192/023 3903
Fax: 023 3275
Email: ntsp@twiga.com
- 4.6.2 Bw. Nasoro Magogo
Forest Herbarium
Tanzania Forest Research Institute
P.O. Box 95
Lushoto
Simu: 027 2645099
Fax: 027 2640187
Email: taforisilvic@twiga.com
- 4.6.3 Bw. Salum Mtou
Small Scale Farmer
Mtanza Msona village
Rufiji District
- 4.6.4 Bw. Bainga Ismail Bwenda
Asst. Agricultural Field Officer
P.O. Box 40, Utete
Rufiji District
Simu: 023 2402972
Email: remputete@twiga.com
- 4.6.5 Prof. Said Iddi
Mkurugenzi wa Misitu na Nyuki
S.L.P. 426
Dar-es-Salaam
Simu: 022 2 126844
Fax: 022 21 30091
Email: misitu@twiga.com
- 4.6.6 Mr. Chande
District Natural Resources Officer
P.O. Box 40, Utete
Rufiji District